JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA


## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI JUNI, 2023

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2023 hali ya ukavu, baridi ya wastani hadi baridi kali ilijitokeza katika maeneo mengi nchini na kusababisha upungufu wa unyevu ardhini, kupungua kwa maji na malisho pamoja na kuwepo kwa hali vumbi. Aidha, hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake inaendana na taarifa ya mwelekeo wa msimu wa Kipupwe (Juni-Agosti), 2023 iliyotolewa mwezi Mei, 2023. Hata hivyo, katika wiki ya nne ya Juni, 2023 vipindi vya upepo mkali pia vilijitokeza na kuathiri baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, kati mwa nchi na nyanda za juu kusini magharibi. Ingawa hali ya ukavu ilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi lakini matukio machache ya mvua kubwa yalionekana katika maeneo ya pwani ya kaskazini, ukanda wa Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki.

### 1.1 Mvua kubwa mwezi Juni, 2023

Katika kipindi cha mwezi Juni 2023, matukio ya mvua kubwa (inayozidi milimita 50 kwa saa 24) yalijitokeza katika maeneo machache nchini. Kituo cha Bukoba kilirekodi kiwango cha juu zaidi cha mvua (milimita 74.3 za mvua) ndani ya saa 24 mnamo tarehe 23 Juni, 2023 ikifuatiwa na Moshi (milimita 56) na Kisiwa cha Pemba (milimita 52.7) mnamo tarehe 1 na 7 Juni, 2023 mtawalia (**Kielelezo 1**). Ripoti kutoka katika vyombo vya habari ilithibitisha kutokea kwa mvua kubwa iliyosababisha athari za mafuriko katika baadhi ya maeneo ya wilaya ya Bukoba (**Kielelezo 2**).




**Kielelezo 1:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Juni, 2023




**Kielelezo 2**: Hali ya Mafuriko iliyowakumba wakazi wa maeneo ya bondeni mjini Bukoba, mkoani Kagera (*Chanzo: Kurasa, EATV*)


### 1.2 Hali joto kwa mwezi Juni, 2023

Kwa kuzingatia hali ya hewa ya muda mrefu (Klimatolojia) kwa mwezi Juni, hakuna hali ya joto kali iliyojitokeza katika kipindi hiki. Hata hivyo, viwango vidogo vya joto la chini vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini (ikiashiria hali ya baridi) ambapo kiwango kidogo zaidi cha joto la chini kilichorekodiwa katika kituo cha Uyole mkoani Mbeya kilikuwa ni nyuzi joto 3.4 °C. Aidha, katika kipindi hiki vituo vya Uyole na Igeri viliripoti viwango vya joto chini ya nyuzi joto 10 °C kwa siku nyingi zaidi ukilinganisha na vituo vingine.Jedwali namba 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo kituo kimerekodi kiwango cha joto la chini cha nyuzi joto 10 °C au chini ya nyuzi joto 10 °C.

Jedwali 1. Viwango vidogo vya joto la chini vilivyojitokeza mwezi Juni, 2023

| Kanda | Kituo | Siku | Kiwango cha Joto la Chini ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| **Nyanda za juu kaskazini mashariki** | Arusha | 1 | ≤ 10 °C |
| **Nyanda za juu kusini magharibi** | Uyole | 26 | ≤ 10 °C |
| | Igeri | 23 | ≤ 10 °C |
| | Iringa | 1 | ≤ 10 °C |
| | Sumbawanga | 6 | ≤ 10 °C |
| **Kanda ya Kusini** | Songea | 2 | ≤ 10 °C |

Kielelezo cha 3 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa kila siku kwa mwezi Juni, 2023 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Kwa ujumla, hali ya baridi kali ilianza kujitokeza katika wiki ya pili ya Juni. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vinaonesha hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya Uyole kuelekea mwishoni mwa mwezi ambapo kiwango cha joto la chini kilipungua zaidi (chini ya nyuzi joto 4°C.)




**Kielelzo 3.** Viwango vya joto la chini kituo cha Uyole na Igeri mwezi Juni, 2023

**1.3 Upepo Mkali**

Katika mwezi huu, vipindi vya upepo mkali unaofika na kuzidi kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba) na maeneo machache ya kati mwa nchi (Singida), magharibi (Tabora) na nyanda za juu kusini magharibi (Songwe). Kasi na nguvu ya upepo ilisababisha ongezeko la vumbi, kupeperusha takataka, mawimbi makubwa ya bahari na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini.

*Imetolewa: tarehe 12 Julai, 2023*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**